

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)**

MALALAMIKO NAMBA. GA.71/135/SHZ/2021/03

SAMSON SANGA.....MLALAMIKAJI

DHIDI YA

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO).....MLALAMIKIWA

TUZO YA MAKUBALIANO

(Imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kupitia waraka wake Na. 23 wa tarehe 23 Novemba, 2021)

1.0 Maelezo ya Awali:

Mnamo tarehe 8 Oktoba 2021, Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji ("EWURA") ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Samson L. Sanga wa Sinde, mjini Mbeya akililalamikia Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania ("TANESCO") (Mlalamikiwa). Mlalamikaji analalamikia kitendo cha Mlalamikiwa kumwekea deni la shilingi 114,392.71 na kumkata kiasi cha pesa kila anaponunua umeme kwa ajili ya matumizi yake ya nyumbani kufidia deni hilo asilolitambua.

Mlalamikaji anaeleza kwamba yeye ni mteja wa Mlalamikiwa wa muda mrefu mwenye mita namba 2421436062. Mlalamikaji anaeleza kuwa alianza kupata uniti pungufu kila anaponunua umeme kutoka kwa Mlalamikiwa kuanzia mwezi 15/06/2021 na alipojaribu kuuliza alijibiwa kuwa kuna makato anakatwa na yeye hayo makato hayatambui. Mlalamikaji

anaendelea kueleza kwamba alipofuatilia kuhusu makato hayo, aligundua kuwa kuna deni la TZS 114,392.71 analokatwa ni la mtu mwingine anayeitwa Simon V. Sanga ambaye ni tofauti na yeye kwani yeye ni Samson L. Sanga. Mlalamikaji pia alieleza kuwa pamoja na kujieleza kwa Mlalamikiwa kuwa hilo deni sio lake bado aliendelea kukatwa deni lisilo halali kila anaponunua umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Hivyo, Mlalamikaji aliamua kuwasilisha Malalamiko yake EWURA na kuiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa kufanya yafuatayo;

- (a) kuondolewa deni lililowekwa kimakosa kwenye akaunti ya mita ya Mlalamikaji; na
- (b) kurudisha fedha zake ambazo Mlalamikiwa amemkata Mlalamikaji kimakosa.

Baada ya kupokea malalamiko ya Mlalamikaji, Mamlaka mnamo tarehe 11 Oktoba 2021 ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuleta majibu ya utetezi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (1) cha Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro. Mnamo tarehe 28 Oktoba 2021, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kukiri kupokea Malalamiko ya Mlalamikaji na kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo;

- (a) Ni kweli kuwa tarehe 15/06/2021 ndugu Samson L. Sanga aliwekewa deni la shilingi 114,392.71 kimakosa. Deni lilipaswa liwekwe kwenye mita ya mteja ajulikanae ndugu Simon Sanga. Pia kutokana na kuingiziwa deni hilo mteja alikatwa shilingi 8,000.00; na
- (b) Mteja huyu alifika ofisini kutoa malalamiko yake na malalamiko yalipokelewa na kufanyiwa kazi ambapo tarehe 22/10/2021 deni lilifutwa kutoka kwenye mita yake namba 24214361602 na kupelekwa kwenye mita sahihi ya Simon Sanga namba ya mita 24219158037. Nakala ya Journal Voucher (JV) No. SS1020 ya tarehe 24/09/2012

imeambatanishwa. Kutokana na kukatwa mteja alitayarishiwa uniti 65 ambazo zitafidia kiasi cha shilingi 8,000.00 alizokatwa.

Kikao cha usuluhishi baina ya pande zote mbili kilifanyika tarehe 4 Novemba 2021 katika ukumbi wa ofisi za EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizopo Mbeya ambapo wadaawa waliafikiana na kukubaliana kama ifuatavyo:

- I. Mlalamikiwa amekubali kuwa kiasi cha shilingi 8,000.00 kilichokatwa kimakosa kutoka kwenye malipo ya Mlalamikaji kitafidiwa kwa kupewa kiasi cha uniti 65 za umeme; na
- II. Uniti hizo 65 zitawekwa kwenye mita ya Mlalamikaji ndani ya saa 48 za kazi kuanzia muda wa muafaka huu.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye '*Kanuni ya 14 (4) ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Taratibu za kutatua Migogoro) Kanuni, Tangazo la Serikali. Namba 428/2020*' na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.


2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kwamba;

- I. Mlalamikiwa amekubali kuwa kiasi cha shilingi 8,000.00 kilichokatwa kimakosa kutoka kwenye malipo ya Mlalamikaji kitafidiwa kwa kupewa kiasi cha uniti 65 za umeme; na
- II. Uniti hizo 65 zitawekwa kwenye mita ya Mlalamikaji ndani ya saa 48 za kazi kuanzia muda wa muafaka huu.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 ' Kanuni 14 (5) ya Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji(Kanuni za kutatua Migogoro) Kanuni, Tangazo la Serikali. Namba 428 la 2020', makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila upande utabeba gharama zake katika shauri hili.

IMETOLEWA KWA LAKIRI ya Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji-EWURA, hapa Dodoma tarehe 23 Novemba, 2021.



.....
KAPWETE LEAH JOHN
KATIBU WA BODI